
Darasa la 1

Kitabu cha hadithi 2

Kiswahili

# ★ Mchezaji Banda

# ★ Kisa cha Simba na Mbuni



Tusome Early Literacy Programme

# Mchezaji Banda

*Mwandishi:* ***Flavia Nanzala***

*Mchoraji:* ***Simon Ndonye***



Huyu ni Banda.

Banda ni mwanafunzi wa darasa la kwanza.

Shule ya Banda inaitwa Hekima.

Banda hupenda kucheza mpira wa miguu.

Banda ni mchezaji shupavu.



Banda ana marafiki wengi.

Juma na Musa ni marafiki wa Banda.

Banda hucheza na marafiki wake.





Banda hucheza mpira vizuri sana.

Banda hufunga mabao mengi.

Banda hushangiliwa akifunga bao.

Jana Banda alicheza mpira.

Banda alianguka na kuumia mkono.

Banda alipelekwa hospitalini kutibiwa.

Alipona na kuendelea kucheza mpira vizuri.



## Maswali

1. Banda ni mwanafunzi wa darasa gani?
2. Banda hupenda mchezo gani?
3. Marafiki wa Banda wanaitwa nani?
4. Banda aliumia wapi?

# Kisa cha Simba na Mbuni

*Mwandishi:* ***Silas Emolem***

*Mchoraji:* ***Simon Ndonye***


Hapo zamani, Simba na Mbuni waliishi pamoja.

Marafiki hawa walikuwa na watoto.

Watoto hao walipendana sana.

Watoto hao walicheza na kula pamoja.





Simba alisema watoto wake walikuwa warembo kuliko wale wa Mbuni.

Mbuni naye alidai watoto wake walikuwa warembo kuliko wale wa Simba.

Simba na Mbuni walibishana siku nyingi.


Waliamua kuwaita wanyama wengine kupiga kura.

Siku ya kura, wanyama walipanga mistari miwili.

Wengine nyuma ya Mbuni na wengine nyuma ya Simba.

Matokeo yalionyesha ushindi ulikuwa ni wa Mbuni.

Wanyama walishangilia na kurukaruka kwa furaha.



Simba alikasirika na kunguruma kwa nguvu.

Alimfukuza Mbuni akitaka kumla.

Wanyama wote waliogopa wakamtoroka Simba.

Baadaye Mbuni alirudi nyumbani na kuwachukua watoto wake.

Walienda nchi ya mbali na kuishi huko bila wasiwasi.

Hadi leo wanyama wengi wakimuona Simba humtoroka.

## Maswali

1. Kwa nini Simba na Mbuni walibishana siku nyingi?
2. Matokeo ya kura ilionyesha ushindi ni wa nani?
3. Ni nini kilimkasirisha Simba?

**Darasa la 1**

Kitabu cha hadithi 2

# ★ Mchezaji Banda

# ★ Kisa cha Simba na Mbuni

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.